**7.0 UTARATIBU ZA KUPATA CHETI CHA KIFO**
Ili kupata cheti cha kifo mwombaji anapaswa kuwasilisha kibali cha mazishi kwa mamlaka ya utendaji wa eneo ambalo tukio la kifo limetokea na kulipa ada ya cheti cha kifo. Ada italipwa kulingana na kiwango kitakachowekwa na Kabidhi Wasii Mkuu.

Kwa mujibu wa sheria, cheti cha kifo cha baba au mama wa familia kitachukuliwa na mwenza aliyebaki au mtoto. Endapo kuna sababu ya msingi inayosababisha washindwe kuchukua cheti hicho, mtu wa karibu wa marehemu anaweza kupokea cheti husika.

**8.0 HITIMISHO**
Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo ni msingi wa upangaji wa maendeleo ya nchi katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.


**Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :**

**Katibu Mtendaji,**
**Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania ,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,**
**Barabara ya Mkalama**
**S.L. P 1718**
**DODOMA**
**TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.go.tz**
**Tovuti: www.rlct.go.tz**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

# USAJILI WA VIFO

**1.0 UTANGULIZI**
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171. Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio na kutathmini utekelezaji wa sharia zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, mwaka 2017 Tume ilifanya mapitio ya sheria zinzohusu usajili wa matukio muhimu ya binadamu ambapo kifo ni miongoni mwa matukio hayo.

**2.0 UMUHIMU WA USAJILI WA TUKIO LA KIFO**
Usajili wa tukio la kifo ni muhimu ili kuwezesha kupatikana kwa cheti cha kifo. Nyaraka hii ni muhimu kisheria ili kuthibitisha kutokea kwa kifo. Uthibitisho huu hutumiwa na familia au ndugu wa marehemu katika kushughulikia masuala ya mirathi. Cheti cha kifo pia kinatumiwa na wanafunzi ambao wamefiwa na wazazi wao wanapoomba mikopo ya elimu ya juu katika Bodi ya Mikopo.

Aidha, usajili wa vifo unasaidia Serikali kwa kuwa inahitaji taarifa na takwimu sahihi za vifo ili iweze kupata takwimu sahihi ya idadi ya watu.

Usajili wa kifo vilevile unaisaidia Serikali kutambua sababu zinazosababisha vifo vya wananchi hivyo kusaidia kuboresha miundo mbinu ya afya na kuchukua hatua mbalimbali za kuzuia vifo hivyo.

**3.0 USAJILI WA TUKIO LA KIFO**
Usajili wa tukio la kifo inasimamiwa na Sheria ya Vizazi na Vifo, Sura ya 108. Sheria imeanisha taratibu za usajii wa tukio la kifo.

**4.0 JUKUMU LA USAJILI WA KIFO**
Sheria imeweka jukumu la kusajili tukio la kifo kwa watu wafuatao:
Daktari aliyethibitisha kifo;
Ndugu wa karibu wa marehemu ambao waliokuwepo wakati wa mwisho wa ugonjwa wa marehemu;
Mmiliki wa nyumba au mkazi wa nyumba, au Mtu yeyote aliyechukua jukumu la kumzika marehemu.

**5.0 MAMLAKA YA USAJILI WA KIFO**
Kabidhi Wasii Mkuu amepewa jukumu la usajili wa vifo. Hata hivyo, sheria imempatia Kabidhi Wasii Mkuu mamlaka ya kukasimisha uandikishaji wa vifo kwa watendaji wafuatao:
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri;
Mtendaji wa Kata, na
Mtendaji wa Mtaa au Kijiji.
Katika kuteleza jukumu hili watendaji wanapokea maelezo katoka kwa Kabidhi Wasii Mkuu.

**6.0 MUDA WA USAJILI WA TUKIO LA KIFO**
Sheria inaelekeza kuwa tukio la kifo lisajiliwe ndani ya siku 30. Hata hivyo, sheria inaruhusu usajili kufanyika baada ya siku 30 usajili huu hutambulika kama usajili uliochelewa.

**6.1 USAJILI WA KIFO NDANI YA SIKU 30**
Sheria inaelekeza kuwa ili kusajili tukio la kifo kilichotokea hospitalini, kituo cha afya au zahanati, mwombaji anatakiwa kuwasilisha kibali cha mazishi kutoka katika sehemu hizo.
Kwa upande wa kifo kilichotokea nyumbani, wahusika wanatakiwa kutoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata, Kijiji, au Msajili wa Wilaya ndani ya siku 30 ili kupata kibali cha mazishi.

**6. 2 USAJI WA KIFO ULIOCHELEWA**
Aina hii ya usajili hufanyika baada ya siku 3 na kuendelea. Ili kufanya usajili uliochelewa, mwombaji anatakiwa kujaza Fomu D3 na kuambatanisha muhtasari wa kikao cha familia na barua inayothibitisha kifo kutoka mamlaka za Serikali zinazohusika, hususan, Ofisi ya Kata au Ofisi Mtendaji wa Kijiji.

Licha ya vielelezo hivyo, mwombaji anapaswa kuwasilisha picha ndogo na kulipa ada itakayoelekezwa na Kabidhi Wasii Mkuu.